TANGAZO LA SERIKALI Na 51J la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI WA KIHANDISI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA KITUO CHA KUHIFADHI KWA WINGI NA UCHAKATAJI WA GESI INAYOTOKANA NA UCHAKATAJI WA MAFUTA GHAFI WA KAMPUNI YA OILCOM YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Huduma ya Ushauri Elekezi wa Kihandisi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kituo cha Kuhifadhi kwa Wingi na Uchakataji wa Gesi Inayotokana na Uchakataji wa Mafuta Ghafi wa Kampuni ya Oilcom ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 3 Julai, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Oilcom kwenye huduma za ushauri elekezi za kihandisi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kituo cha Kuhifadhi kwa Wingi na Uchakataji wa Gesi inayotokana naUchakataji wa Mafuta Ghafi inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2026 kwa mujibu wa kipengele cha 3.3 cha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Oilcom na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31/12/2024

**MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
*Waziri wa Fedha*